



SYRACUSE CITY SCHOOL DISTRICT

Jaime Alicea, Superintendent of Schools

Huduma za Afya

Dk. Ted Triana, Mkurugenzi wa Huduma za Afya

03/04/2020

Mpendwa Mzazi/Mlezi:

Huku idadi ya watu waliogunduliwa kuwa na virusi vya korona (COVID-19) katika jimbo la New York ikiendelea kupanda nilitaka kushiriki nawe taarifa fulani. Hatari kwa wanafunzi na familia zetu kuambukizwa COVID-19 bado iko chini ingawa hatutarajii kuwa idadi ya watu waliogunduliwa kuwa na virusi itaendelea kupanda. Kwa sasa, hakuna ripoti za mtu yeyote aliye na virusi katika Kaunti ya Onondaga.

Onondaga County Health Department (Idara ya Afya ya Kaunti ya Onondaga) inajiandaa kwa uangalifu kwa matukio yote yanayoweza kutokea endapo watu wataambukizwa humu. Katika Syracuse City School District tutaendelea kufuata mapendekezo kutoka Idara ya Afya ya Kaunti ya Onondaga, New York State Department of Health (Idara ya Afya ya Jimbo la New York) na Center for Disease Control (Kituo cha Kudhibiti Magonjwa) huku tukifuatilia athari yoyote inayowezekana inayohusisha jamii yetu ya shule.

Tumeanzisha itifaki za ziada za usafi kwenye shule na ofisi zetu zote. Vilevile, tunaendelea kupigia debe kunawa mikono vizuri huku tukihimiza wale wanaougua kusalia nyumbani. Desturi hizi zinapendekezwa kupunguza uenezaji wa ugonjwa.

Wanafunzi, familia na wafanyakazi wote wa SCSD wanapaswa kuendelea kuchukua hatua za jumla za kuzuia homa ili kupunguza uenezaji wa magonjwa ya kupumua ikiwa ni pamoja na COVID-19. Hizi ni pamoja na:

- Kufumba kikohozi au chafya yako kwa shashi au mkono wa vazi
- Kunawa mikono yako mara kwa mara
- Kuepuka kuugusa uso wako
- Kuepuka mgusano wa karibu na watu wanaougua
- Kuangamiza viini kwenye sehemu zinazotumika mara kwa mara (vitasa vya nungu/nundu, simu, n.k.)
- Kupata chanjo ya homa – hakuna muda usiofaa
- Kusalia nyumbani ikiwa unajihisi kuwa mgonjwa. Kuwasiliana na daktari wako na kumfahamisha dalili zako na historia ya safari.


Ikiwa mtoto wako ataugua akiwa shuleni au kuwasili shuleni akiwa na dalili kama za homa, atapewa barakoa na utahitajika kumchukua kutoka shuleni kama tahadhari. Tafadhali wasiliana na mtoa huduma ya afya wa mtoto wako inavyohitajika kwa ajili ya ugonjwa alio nao.

Rasilimali za Ziada:

- Tovuti mahususi ya CDC kuhusu 2019-nCoV kwenye <https://www.cdc.gov/nCoV>.
- Tovuti mahususi ya NYSDOH kuhusu 2019-nCoV kwenye <https://www.health.ny.gov/diseases/communicable/coronavirus/>
- Idara ya Afya ya Kaunti ya Onondaga: <http://www.ongov.net/health/coronavirus.html>
- Maelezo ya idara za afya za karibu ya NYSDOH https://www.health.ny.gov/contact/contact_information/
- Tovuti ya New York State Center for School Health kwenye www.schoolhealthny.com

Tutaendelea kuwasiliana na jamii ya SCSD kuhusu jitihada zetu tunazoendeleza kuhusu virusi vya korona.

Wako mwaminifu,



Dk. Ted. J. Triana, D.O.
Mkurugenzi wa Matibabu wa SCSD

TT/sm